**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

# TAARIFA KWA UMMA KUHUSU NAFASI ZA AJIRA MBADALA KWA WALIMU WA SHULE ZA MSINGI NA SEKONDARI NA WATUMISHI WA KADA MBALIMBALI ZA SEKTA YA AFYA

**Ndugu Wanahabari,**

Ofisi ya Rais - TAMISEMI inapenda kuutangazia Umma kuwa Serikali imetoa kibali cha Nafasi za Ajira ya **Walimu 6,949** wa Shule za Msingi na Sekondari na **Watumishi 2,726** wa Kada mbalimbali za Sekta ya Afya ili kujaza nafasi wazi za watumishi waliokoma utumishi kutokana na sababu mbalimbali kama vile vifo, kuacha kazi, kufukuzwa kwenye utumishi na kustaafu.

Kwa sababu hiyo, nachukua fursa hii kuutangazia umma kuwa taratibu za kuanza mchakato wa kuomba ajira hizo umekamilika na kwamba waombaji wote wenye nia ya kuomba ajira wanaweza kutuma maombi yao kwa njia ya mtandao kupitia kiunganishi cha ***ajira.tamisemi.go.tz*** kuanzia tarehe **09/05/2021** hadi **23/05/2021**.

**Ndugu Wanahabari,**

Waombaji wanaotakiwa kutuma maombi ni wenye sifa za kitaaluma kama ifuatavyo:

## 1.0 SEKTA YA ELIMU:

### 1.1 WALIMU WA SHULE ZA MSINGI:

Walimu wanaoomba kuajiriwa kufundisha Shule za Msingi wawe na sifa zifuatazo:-

i) **Mwalimu Daraja la IIIA:** Mhitimu wa Astashahada ya Ualimu Elimu ya Msingi, Astashahada ya Ualimu Elimu ya Michezo, Astashahada ya Ualimu Elimu ya Awali;

ii) **Mwalimu Daraja la IIIB:** Mhitimu wa Stashahada ya Ualimu wa Elimu ya Awali, Stashahada ya Ualimu wa Elimu ya Msingi na Stashahada ya Ualimu wa Elimu Maalum; na

iii) **Mwalimu Daraja la IIIB:** Mhitimu wa Stashahada ya Ualimu katika masomo ya English Language, History na Geography.

## 1.2 WALIMU WA SHULE ZA SEKONDARI:

i) **Mwalimu Daraja la IIIB:** Mhitimu wa Stashahada ya Ualimu wa masomo ya Physics, Mathematics, Biology na Chemistry;

ii) **Mwalimu Daraja la IIIC:** Mhitimu wa Shahada ya Ualimu aliyesomea Elimu Maalum kwa masomo ya Physics, Chemistry, Biology, Mathematics;

iii) **Mwalimu Daraja la IIIC:** Mhitimu wa Shahada ya Ualimu wa masomo ya Physics, Mathematics, Chemistry na Biology; na

iv) **Mwalimu Daraja la IIIC:** Mhitimu wa Stashahada ya Uzamili katika Elimu (Post Graduate Diploma in Education) lazima awe mwenye Shahada ya Kwanza (Bachelor Degree) yenye masomo yaliyotajwa katika (ii) na iii) hapo juu.

## 1.3 WAHITIMU WALIOSOMA NJE YA NCHI:

i) Waombaji wote waliosoma Elimu ya Sekondari nje ya Nchi wanatakiwa kupata Namba ya Ulinganifu wa Matokeo *(Equivalent Number)* inayoanza na Herufi **EQ…** kutoka Baraza la Mitihani la Tanzania ili kuwawezesha kuingia kwenye Mfumo wa Ajira; na;

ii) Waombaji waliosoma Vyuo Nje ya Nchi wanatakiwa kupata Ithibati ya masomo yao kutoka Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU) ili Vyeti vyao viweze kutambuliwa na kupata uhalali wa kutumika hapa Nchini.

## 1.4 SIFA ZA JUMLA ZA MWOMBAJI:

Mwombaji wa nafasi zilizoainishwa hapo juu awe na sifa za jumla zifuatazo: -

i) Awe ni Mtanzania;

ii) Awe na Umri usiozidi miaka arobaini na tano (45)

iii) Awe hajawahi kufukuzwa, kuacha kazi au kustaafishwa katika Utumishi wa Umma isipokuwa kwa kibali cha Katibu Mkuu Kiongozi.

iv) Awe na Namba ya Kitambulisho cha Taifa.

v) Waombaji wenye Shahada na Stashahada za NACTE na TCU (UDOM) waambatishe Cheti cha kuhitimu mafunzo na “Transcript”. Waombaji wa Astashahada na Stashahada za NECTA waambatishe Cheti cha Mafunzo katika sehemu mbili *(weka Cheti na weka “Transcript”)* na;

vi) Walimu wenye Ulemavu wenye sifa zilizoainishwa sawa na Tangazo hili, watume maombi yao ya kazi kwa nakala ngumu *(hard copy)* kwa EMS. Maombi yao yaeleze aina ya Ulemavu wao na kuambatisha picha zao na yatumwe kwa anuani ifuatayo:-

Katibu Mkuu,
Ofisi ya Waziri Mkuu,
S.L.P. 980,
**40480 DODOMA** ***(Aione: Mkurugenzi wa Kitengo cha Watu Wenye Ulemavu)***

## 2.0 SEKTA YA AFYA:

2.1 Daktari Daraja la II

2.2 Daktari wa Meno Daraja la II

2.3 Tabibu Daraja la II

2.4 Tabibu Msaidizi

2.5 Tabibu wa Meno Daraja la II

2.6 Tabibu Meno Msaidizi

2.7 Mfamasia Daraja la II

2.8 Mteknolojia (Dawa) Daraja II

2.9 Mteknolojia Msaidizi (Dawa)

2.10 Mteknolojia (Maabara) Daraja II

2.11 Mteknolojia Msaidizi (Maabara)

2.12 Mteknolojia (Mionzi) Daraja II

2.13 Mteknolojia (Macho) Daraja II

2.14 Afisa Muuguzi Daraja la II

2.15 Afisa Muuguzi Msaidizi Daraja la II

2.16 Muuguzi Daraja la II

2.17 Mtoa Tiba kwa Vitendo Daraja la II

2.18 Afisa Afya Mazingira Daraja la II

2.19 Afisa Afya Mazingira Msaidizi Daraja la II

2.20 Msaidizi wa Afya

2.21 Katibu wa Afya Daraja la II

2.22 Afisa Ustawi wa Jamii Daraja la II

2.23 Afisa Lishe Daraja la II

**3.0 SIFA ZA WAOMBAJI KWA UJUMLA:**

i) Awe Raia wa Tanzania;

ii) Awe na Umri usiozidi miaka 45;

iii) Awe na namba ya Kitambulisho cha Taifa;

iv) Awe na Vyeti kamili vya Mafunzo ya Fani aliyosomea;

v) Asiwe mwajiriwa wa Serikali au asiwe mwajiriwa wa Hospitali za Mashirika ya Dini ambaye Mshahara wake unalipwa na Serikali; na

vi) Asiwe mwajiriwa wa Serikalini au amewahi kuajiriwa Serikalini

**4.0 MAOMBI YOTE YAAMBATISHWE NA NYARAKA ZIFUATAZO:**

i) Nakala ya Cheti cha Kidato cha Nne/Sita;

ii) Nakala za Vyeti vya Taaluma;

iii) Nakala ya Cheti cha Kuzaliwa;

iv) Nakala ya Cheti cha Usajili kamili (*Full Registration*) au Leseni ya kufanya kazi ya taaluma husika;

v) Awe na namba ya Kitambulisho cha Taifa; na

vi) Maelezo Binafsi (CV), yakionesha Umri, Anuani kamili na Namba ya Simu ya kiganjani, pamoja na Anuani/Namba za Simu za kiganjani za wadhamini wasiopungua wawili.

## 5.0 MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA KWA WAOMBAJI WOTE:

i) Waombaji wote wawe tayari kufanya kazi katika Halmashauri watakazopangiwa;

ii) Waombaji wawe tayari kufanya kazi na Mashirika au Taasisi zilizoingia Ubia na Serikali;

iii) Waombaji waliosoma Nje ya Nchi wanatakiwa waambatishe *"Equivalent Certificate"* kutoka NECTA/NACTE/TCU; na

iv) Mara baada ya kupangiwa Kituo cha kazi, hakutakuwa na nafasi ya kubadilishiwa Kituo cha kazi.

## 6.0 MWISHO

Maombi yote ya ajira yatumwe kupitia kwenye mfumo wa maombi ya ajira wa Ofisi ya Rais – TAMISEMI kama ulivyooneshwa kwenye Tangazo hili. Hakuna maombi yatakayopokelewa kwa njia tofauti na iliyoelekezwa **isipokuwa kwa Waombaji wenye Ulemavu.** Waombaji wanatakiwa kutuma maombi yao kuanzia tarehe **09/05/2021** hadi **23/05/2021**.

Pamoja na maelezo kuhusu utaratibu wa kutuma maombi, Kituo cha Huduma kwa Wateja cha Ofisi ya Rais – TAMISEMI kitakuwa wazi kuanzia Saa 1.30 Asubuhi hadi Saa 12.00 jioni kwa kipindi chote cha kuwasilisha maombi. Hatua hiyo inalenga kusaidia waombaji watakaohitaji maelezo au ufafanuzi zaidi katika kukamilisha maombi yao. Kwa mawasiliano na Kituo cha Huduma kwa Wateja tumia Namba za Simu: **026 2160210** na **0735 160210.**

Kwa taarifa hii, Halmashauri zote zinaelekezwa kujiandaa kupokea Watumishi wapya ikiwemo kutenga fedha za kujikimu na stahiki nyinginezo kwa Watumishi wa ajira mpya kwa **Kada ya Afya.**

Ummy A. Mwalimu (Mb.)

**WAZIRI WA NCHI**

**OFISI YA RAIS – TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**09 Mei, 2021**